

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAMISEMI

**Namba za Simu:**

**Mkuu wa shule:**
**0767826144/0755665995**

SHULE YA SEKONDARI MWANDIGA
S.L.P 389
**KIGOMA**
11.05.2018

**KUMB.NA.MWSS/S.386/J.28/2018**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi…………

S.L.P……………………………………

…………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWANDIGA HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA MKOA WA KIGOMA MWAKA 2018.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2018. Shule ya sekondari Mwandiga ipo umbali wa kilometa 10 kaskazini mwa mji mkuu wa Halmashauri/mkoa. Usafiri wa basi kutoka mjini Kigoma unapatikana katika kituo cha mabasi Kigoma nauli ni shilingi 400/=.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe 02/07/2018. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kati ya tarehe 30/06/2018 na tarehe 01/07/2018 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 16/07/2018.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare ya Shule (WAVULANA).

a) Mashati mawili meupe mikono mirefu yenye ukosi (kola)
b) Suruali mbili rangi ya bluu kali (Dark blue) zenye malinda na zisiwe za kubana. (model)
c) Viatu vyeusi vya ngozi na soksi nyeusi.
d) Viatu vya raba kwa ajili ya michezo na Trucksuit ya kijani yenye mistari ya manjano.
e) T-shirt rangi ya bluu zinapatikana shuleni kwa gharama nafuu. Nunua T-shirt moja ya rangi ya kijani isiyo na maaandishi wala picha ya kushindia.
f) Sweta rangi ya bluu aje nalo
g) Tai ya rangi ya dark blue.

**NB:** Usije na nguo za nyumbani.

3. **ADA NA MICHANGO YA SHULE**

Ada ya shule kwa mwaka ni 70,000/= unaweza kulipa 35,000/= kwa kila muhula, vile vile ada inalipwa moja kwa moja Benki ya NMB A/C 51601100067 akaunti ni Mwandiga sekondari usisahau kuandika jina la mwanafunzi aliye lipa ada juu ya pay slip ili kuweka kumbukumbu ya malipo ya ada afikapo shule.

Michango inayo takiwa kulipwa na mzazi ni:

(i) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
(ii) Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho
(iii) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
(iv) Shilingi 30,000/= wapishi, walinzi na vibarua wengine
(v) Shilingi 2000/= nembo ya shule
(vi) Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza, Tsh 5000/= na Bima ya afya Tsh 5000/= (wanafunzi washauriwe kujiunga na mfuko wa Bima ya Afya CHF kikaya)
(vii) Fedha ya tahadhali Tsh 5000/= (Haitarejeshwa)
(viii) Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima MOCK.

**ANGALIZO**: Jumla ya michango na Ada kwa wanafunzi ni Tsh 178,000/= ilipwe katika akaunti na NMB A/C 51601100067 Jina la akaunti Mwandiga Sekondari , Jina la mwanafunzi aliye lipa liandikwe juu ya pay slip kwa kumbukumbu.

4. **MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI.**

(i) Ream ya karatasi 1 A4 (kwa Mwaka)
(ii) Godoro kwa wanafunzi wa bweni futi 2.5 kwa 6.
(iii) Mashuka, blanketi, mito, foronya (blue/pinki)
(iv) Vyombo vya kulia (visivyo vya inta)
(v) Picha za passport mbili
(vi) Ndoo mbili ndogo
(vii) Jembe, kwanja, mopa, mifagio ya ndani na nje.
(viii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
(ix) Scientific calculator.
(x) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biologia

5. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

(i) Wizi
(ii) Kutokuhudhuria shule ama masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla
(v) Kupigana wanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au yeyote yule
(vi) Ulevi na unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya
(vii) Uvutaji wa sigara
(viii) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
(ix) Kujihusisha na masuala ya siasa shuleni

(x) Kumiliki silaha kama visu, panga bwenini

(xi) Kutembelea ama jumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(xii) Kumiliki simu ya mkononi shuleni

(xiii) Kudharau Bendera ya Taifa

(xiv) Kufanya jaribio lolote la kujiua kama kunywa sumu n.k

(xv) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

(xvi) Kujiunganishia umeme kienyeji kwenye mabweni, bwalo darasa.

6. MAMBO MENGINE MUHIMU
   (A) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali Fomu hii imeambatanishwa na barua hii.
   (B) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi mkataba wakutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
   (C) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine ya yatayotolewa na shule.
7. Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.......................................................

ALBERT A. MUTWE THE HEADMASTER

MWANDIGA SEC. SCHOOL

P.O. BOX 389

KIGOMA

MKUU WA SHULE.

*FORM A*

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**
**MWANDIGA HIGH SCHOOL**
**P.O. BOX 389 KIGOMA.**

(To be completed by a Medical Officer in respect of all Form One/ Five entrants).

Full Name.......................................................................................................................
Age.............................................................. Sex ..................................................
Blood count (red or white) ...........................................................................
Stool examination ......................................................................................
Urine analysis .............................................................................................
T.B Test ......................................................................................................
Ears ...........................................................................................................
Chest ..........................................................................................................
Eye .............................................................................................................
Spleen .........................................................................................................
Abdomen .....................................................................................................
Pregnancy test .............................................................................................

ADDITIONAL INFORMATION e.g. physical defects or impairment (s) infection chronic of family diseases.
.......................................................................................................................
.......................................................................................................................
.......................................................................................................................

I certify that the above is fit to pursue as stated above.

Signature....................................................................
Designation ...............................................................

Date................................................. Station .....................................................................

**NOTE**: Medical officer. At the time of examination please tress the individual for any ailments.

**NB:** This completed form should be sent to the school with acceptance from or brought when you come to school. No pupil may enroll without certificate of physical fitness.

*FOMU B*

**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

Jina la mwanafunzi.........................................................................................................................

Anuani ya nyumbani...........................................................................................................................

Kabila........................................umri/mwaka wa kuzaliwa..............................................................

Jina la Baba ....................................................... (Hai/marehemu) mwaka aliofariki.......................

Dini ..................................................Kazi..........................................................................................

Jina la mama ..................................................(Hai/marehemu) mwaka aliofariki...........................

Dini.....................................................Kazi.........................................................................................

Nd gu wengine wanaohusishwa na masuala ya mwanafunzi iwapo wazazi hawapo.

| NA | JINA | UMRI | UHUSIANO |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |

Jina la mzazi/mlezi unayemtegemea...................................................................................................

Anuani.............................................................................................................................................
.

............................................................ ............................................................

............................................................ ............................................................

Sahihi na jina la mwanafunzi    Sahihi na jina la mzazi/mlezi

FORM C

KARATASI HII IJAZWE NA MZAZI AU MLEZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

Mimi (Bw/Bibi/Bi............................................................................................

Mzazi/mlezi wa ...................................................................... Nimesoma na kuelewa Barua ya Mkuu wa Shule ya sekondari Mwandiga kuhusu masharti ya kujiunga na shule. Nimezungumza na mwanangu.................................................... ......................................................Ameahidi kuyatekeleza masharti na atafuata sheria za shule. Ninakubali/sikubali mtoto wangu apewe nafasi katika shule ya sekondari ya Mwandiga. Mtoto wangu akiwa shuleni alelewe katika dini ya ..........................................................................

..................................................

Sahihi ya mzazi/mlezi